

MUNGU AMENITEUA NILIHUBIRI

Alfred Ogombo

1. Mu-ngu a-me-ni - te - u - a ni-li hu-bi-ri ni wa - ji-bu wa-ngu
Kwa ma ta - i - fa mba - li mba-li ma - ta - i - fa ne-no na li - pe - nye

Kitikio

ku-li-hu-bi - ri ne-no Ma - fu - ndi-sho ya Bwa - na ni nga - o
ko - te li - pe - nye ko - te Ma - fu - ndi-sho ha - ya ha - ki - ka ni

ya-ngu mi-mi ni wa - po vi - ta-ni dhi-di ya she-ta - ni
ta - a ya-ngu ku - a - nga - za nji-a ya ku - fua-ta mi-mi

2. Neno lake Bwana ndugu halibagui, kwani sote tuko sawa mbele ya Mungu
Analotaka Bwana tunyenyekee, tumakinike tulisikize neno

3. Neno lake Bwana limejaa msamaha, tumaini la uzima sote twapata
Vile yatupasa kuishi maisha yetu, Biblia ndilo mwongozo kamili

4. Neno la hekima ndilo neno la Bwana, neno la wokovu ndilo neno la Bwana
Neno la uponyaji ndilo neno la Bwana, neno la uhuru ndilo neno la Bwana

5. Akina baba wote msikie neno, akina mama wote msikie neno
Nao vijana wote msikie neno, nanyi watoto wote msikie neno